4.0 KISWAHILI (102)

MANYAM FRANCHISE
DiscoverILearnIApply

4.1 MATOKEO YA MTIHANI WA SOMO LA KISWAHILI MWAKA WA 2010

Jedwali hili linaonyesha matokeo ya mtihani wa somo la Kiswahili katika muda wa miaka minne (2007 hadi 2010).

Jedwali 4: Matokeo ya mtihani wa Kiswahili (2007 – 2010)

Mwaka	Karatasi	Watahiniwa	Alama ya Juu	Alama ya Wastani	Alama ya Tanganisho
2007	1		40	15.80	6.42
	2		80	32.22	11.91
	3		80	43.49	13.12
	Jumla	**272,905**	**200**	**91.51**	**27.00**
2008	1		40	14.20	7.18
	2		80	29.18	11.43
	3		80	31.17	13.64
	Jumla	**304,314**	**200**	**74.55**	**32.25**
2009	1		40	15.40	6.93
	2		80	29.03	11.96
	3		80	32.72	13.11
	Jumla	**335,377**	**200**	**77.15**	**32.00**
2010	1		40	14.32	6.53
	2		80	33.77	11.96
	3		80	39.22	14.09
	Jumla	**354,738**	**200**	**87.10**	**28.73**

Jedwali hili laonyesha kuwa kwa ujumla:

4.1.1 Alama ya wastani ya karatasi ya 1(102/1) ya mwaka wa 2010 imeshuka ikilinganishwa na mwaka wa 2009.

4.1.2 Matokeo ya karatasi ya pili (102/2) ya mwaka wa 2010 yameshuka yakilinganishwa na yale ya mwaka wa 2009.

4.1.3 Matokeo ya karatasi ya tatu (102/3) ya mwaka wa 2010 yameimarika kutoka alama ya wastani **32.72** mwaka wa 2009 hadi **39.22** mwaka wa 2010.

4.1.4 Matokeo ya Kiswahili kama somo kwa jumla katika mwaka wa 2010 yameimarika. Alama ya wastani ya Kiswahili kama somo mwaka huu ni **87.10** yakilinganishwa na mwaka wa 2009 ambapo alama hii ilikuwa **77.15**(ongezeko la **10.16**)

Alama ya tanganisho inaonyesha kuwa kuna baadhi ya watahiniwa ambao waliweza kujipatia alama nyingi zaidi ya alama ya wastani mwaka wa 2010, ikilinganishwa na mwaka 2009. Alama hii ilikuwa **32.58**.

4.2 INSHA (102/1)

Jedwali 5: Matokeo ya Karatasi ya kwanza ya miaka ya 2007 – 2010.

Mwaka	2007	2008	2009	2010
Alama ya Wastani	15.80	14.20	15.40	14.32
Alama ya Tanganisho	6.42	7.18	6.93	6.53

Jedwali hili laonyesha kwamba kwa miaka hii minne (2007-2010), matokeo ya karatasi ya 102/1 yamekuwa yakipanda na kuteremka na kwamba watahiniwa wengi hawajaweza kujipatia alama zaidi ya nusu ya alama zote ambazo zinaweza kutuzwa ambazo ni 40. Katika mwaka wa 2010, matokeo haya yaliteremka kwa kiasi cha alama **1.08.**

Powered By: www.manyamfranchise.com

Tutachanganua swali la kwanza ambalo lilikuwa la lazima na ambalo halikufanywa vizuri.

Swali la 1

> Andika wasifu wa ndugu yako ambaye amepanga hafla ya kuchangisha pesa za kumgharamia masomo ya Chuo Kikuu.

Watahiniwa walikosa alama kwa sababu wengi hawakutofautisha kati ya wasifu, wasifukazi, wasifutanzia, tawasifu,ratiba,barua,kumbukumbu na kadhalika.

*Tafadhali tazama mwongozo ulioambatanishwa katika ripoti hii ili uone jinsi insha hii ya hotuba ilivyostahili kuandikwa.

USHAURI KWA WALIMU
-Walimu wawatayarishe wanafunzi wao katika maeneo yote bila ubaguzi kama ilivyo katika silabasi ya Taasisi ya Elimu.

4.3 MAPENDEKEZO:

-Walimu wazidi kuwapa wanafunzi mazoezi zaidi katika uandishi wa kiuamilifu.
-Walimu watumie silabasi za K.I.E na K.N.E.C katika ufundishaji wao.
-Wanafunzi wahimizwe kusoma magazeti na kujifahamisha na matukio ya kila siku katika jamii na mazingira yao-kitaifa na pia kimataifa; ilmuradi waweze kuyashughulikia maswali yanayohusu masuala ibuka iwapo yatatahiniwa.
Haitoshi kujifunga katika masuala yaliyo vitabuni pekee.
-Wanafunzi waamasishwe kutafsiri maswali kwa uangalifu mkubwa huku wakizingatia maneno muhimu.

4.4 LUGHA (102/2)

Jedwali 6: Matokeo ya Karatasi ya pili (102/2) ya miaka ya 2007 hadi 2010.

Mwaka	**2007**	**2008**	**2009**	**2010**
Alama ya Wastani	32.22	29.18	29.03	33.77
Alama ya Tanganisho	11.91	11.43	11.96	14.09

Matokeo ya karatasi ya 102/2 yameimarika mwaka wa 2010. Matokeo haya ndiyo bora zaidi katika kipindi cha miaka minne.

Maswali ya ufahamu na ufupisho/muhtasari ndiyo yaliyowatatiza watahiniwa.
Tutayachanganua hapa.

Swali la 1

Powered By: www.manyamfranchise.com

1 **UFAHAMU** (alama 15)

Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali

Suala la mahusiano ya wanadamu katika jamii, uainishaji wake na udhihirikaji wake limewashughulisha wataalamu wa elimu jamii kwa dahari ya miaka. Suala hili huwatafakarisha wataalamu hao kutokana na umuhimu wake katika maisha ya binadamu. Msingi mkuu wa uainishaji wa mahusiano hayo ni kukichuza kipindi cha mahusiano yenyewe. Yapo mahusiano baina ya waja ambayo yanachukua muda mfupi, kwa mfano saa au dakika chache, na mengine ambayo huenda yakachukua miaka ayami.

Mahusiano ya muda mrefu kabisa ni yale yanayojulikana kama mahusiano ya kudumu. Inamkinika kudai kuwa miundo ya kijamii, kisiasa na kiuchumi huweza kuyadhibiti mahusiano hayo kwa kiasi kikubwa. Watu wengi huitakidi kuwa uhusiano uliopo baina ya mtu na jamaa yake utachukua muda mrefu, na kwa hiyo ni uhusiano wa kudumu. Hali hii hutokana na uhalisi kuwa tunahusiana na jamaa zetu kwa kipindi kirefu labda tangu ukembe hadi utu uzima wetu. Uhusiano huu hautarajiwi kuvunjwa na umbali wa masafa baina yetu; tunaendelea kuwasiliana kwa barua au, katika enzi hii ya utandawazi, kwa kutumia nyenzo za teknohama kama mtandao na simu za mkononi, na kudumisha uhusiano wetu wa kijamaa. Hata hivyo, inawezekana baadhi ya mahusiano ya kijamaa yasiwe ya kudumu. Mathalan, uhusiano uliopo baina ya mke na mume, na ambao unatarajiwa kuwa wa kudumu au wa kipindi kirefu, unaweza kuvunjwa kwa kutokea kwa talaka. Talaka hiyo inavunja ule uwezekano wa uhusiano wa kudumu unaofumbatwa na sitiari ya pingu za maisha.

Katika ngazi ya pili, mahusiano ya kipindi cha wastani, kuna mahusiano yanayohusisha marafiki zetu maishani, shuleni au kwenye taasisi zozote zile, majirani zetu, wenzetu katika mwahali mwa kazi, washiriki kwenye sehemu za ibada au za burudani na wenzetu kwenye vyama tofauti na makundi ya kujitolea. Inawezekana kudahili kuwa baadhi ya mahusiano haya, hususan baina ya marafiki na majirani huweza kuwa ya miongo na daima. Hali hii huweza kutegemea muundo na mfumo wa jamii. Kwa mfano, kwa wanajamii wanaoishi kwenye janibu fulani mahsusi, na kwa miaka tawili bila ya kuhajiri, uhusiano wao na majirani huweza kuwa wa kudumu. Hali hii **inasigana** na hali iliyoko kwenye maisha ya mijini. Maisha ya mijini yana sifa ya kubadilikabadilika. Isitoshe, kutokana na mfumo wa maisha ya kibepari **yameghoshi** ubinafsi mwingi. Mawimbi ya mabadiliko na ubinafsi huweza kuumomonyoa ukuta wa uhusiano wa kudumu.

Mwelekeo wa maisha ya siku hizi ya uhamaji kutoka maeneo au viambo walikoishi watu unasababisha kupombojea kwa mahusiano ya kudumu baina yao na majirani zao. Uhusiano kati ya wenza katika mazingira ya kazi unahusiana kwa kiasi fulani na ule wa majirani. Vimbunga vya ufutwaji kazi, ubadilishaji wa kazi, hali zisizotegemewa na mifumo ya kimataifa pamoja na hata mifumo ya kisiasa huweza kuathiri mshikamano wa wanaohusika kazini.

Kiwango cha mwisho cha mahusiano ni uhusiano wa mpito au wa muda mfupi. Mahusiano ya aina hii hujiri katika muktadha ambapo pana huduma fulani. Huduma hizi zinaweza kuwa za dukani, kwenye sehemu za ibada, kwenye kituo cha mafuta, kwa kinyozi, kwa msusi na kadhalika. Kuna sababu kadha zinazotufanya kuyazungumzia mahusiano ya aina hii kama ya mpito. Kwanza, uwezekano wa mabadiliko ya anayeitoa huduma hiyo ni mkubwa. Si ajabu kuwa unaporudi kwa kinyozi au msusi unatambua aliyekushughulikia hayupo. Hata hivyo, kuna **vighairi** hususa pale ambapo mtoa huduma anayehusika ni yule yule mmoja.

Mahusiano ya mpito yanatawaliwa na 'uhusiano wa chembe chembe.' Uhusiano wa chembe chembe, bidhaa ya mfumo wa kibepari, unamaanisha kuwa kinachomshughulisha mtu ni chembe ndogo tu ya mwenzake. Chembe hiyo inaweza kuwa huduma, kwa mfano, gazeti analokuuzia mtu, viatu anavyokushonea, nguo anazokufulia, ususi anaokufanyia n.k. Mahusiano ya aina hii yametovukwa na hisia za utu na ni zao la mifumo ya kisasa ya kiuchumi na kijamii. Mtu anayehusiana na mwezake kwa misingi ya chembe ndogo tu, huenda asijali kama mwenzake amekosa chakula, amefutwa kazi, amefiliwa, ameibiwa na kadhalika.

Suala kuu tunalopaswa kujiuliza ni: je, tunahusiana vipi na jamaa zetu, taasisi zetu, marafiki zetu na majirani zetu? Je, uhusiano wetu na raia wenzetu ni wa aina gani? Je, uhusiano wetu na nchi yetu ni wa mpito au ni wa kudumu?

- Kwa ujumla, maswali ya kifungu yalihitaji mtahiniwa asome, aelewe na kuchanganua, kusanisi, kutafsiri, kutathmini na kutumia maudhui katika kifungu kujibu maswali.

- Watahiniwa pia walikosa alama katika swali hili kwa sababu wengi hawakuwa na stadi ya kujieleza vizuri na wakafanya makosa mengi ya sarufi na tahajia.

(a) Taja kigezo muhimu cha kuzungumzia mahusiano. (alama 1)

Powered By: www.manyamfranchise.com

(b) Eleza imani ya watu kuhusu uhusiano baina ya jamaa. (alama 1)

(c) Fafanua athari ya teknolojia kwenye mahusiano ya watu. (alama 2)

(d) Eleza sababu nne kuu za kuharibika kwa mahusiano katika maisha ya leo. (alama 4)

(e) Taja sifa kuu ya mahusiano ya muda mfupi. (alama 2)

(f) Je, kifungu, hiki kina ujumbe gani mkuu? (alama 2)

Majibu

(a) Kukichungua au kukiangalia kipindi cha mahusiano yenyewe.

(b) Kuwa utakuwa uhusiano wa kudumu/utakuwa uhusiano wa muda mrefu.

(c) Huwezesha watu au jamaa walio mbali kuwasiliana/simu au mtandao huwa chanzo au nyenzo muhimu ya kudumisha uhusiano.

(d) Mabadiliko ya mara kwa mara/kuwepo kwa ubinafsi mwingi.
- Uhamaji wa watu kutoka viambo/mitaa yao
- Ufutwaji wa watu kazini na kwa hivyo kutengana na wenzao.
- Ubadilishaji wa kazi.
- Kutotegemeka kwa kazi zenyewe.
- Nguvu na kani za kiuchumi ni nyingi.
- Mifumo ya kisiasa huweza kuathiri maisha.

(e) Uhusiano wa chembechembe/mtu hujihusisha na chembe ndogo ya mwenzake.
Mahusiano yanapasa kutawaliwa na hisia za utu, undani – yaani mahusiano yanayogusa nafsi zetu,ya dhati, ya kuwajibika kwa wenzetu na nchi yetu.

(f) (i) Inapingana;
(ii) yamejaa/yametawaliwa na
(iii) vinyume

Powered By: www.manyamfranchise.com

Swali la pili: UFUPISHO/MUHTASARI

2 MUHTASARI (alama 15)

Jamii ya leo inatawaliwa na kuendeshwa na kanuni ya maarifa. Inawezekana kusema kuwa uchumi wa jamii za leo na zijazo utategemea maarifa zaidi kuliko utakavyotegemea wenzo wowote mwingine. Utambuzi wa uwezo mkubwa wa maarifa katika maisha ya binadamu ndio msingi wa watu kusema 'maarifa ni nguvu.'

Maarifa huelezwa kwa tamathali hii kutokana na uwezo wa: kuyadhibiti, kuyaendesha, kuyatawala na kuyaongoza maisha ya binadamu popote pale walipo. Mtu ambaye ameyakosa maarifa fulani huwa ameikosa nguvu hiyo muhimu na maisha yake huathirika pakubwa. Kwa msingi huu, maarifa yanaweza kuangaliwa kama utajiri mkubwa ambao binadamu anaweza kuutumia kwa faida yake au kwa faida ya wanajamii wenzake. Ukweli huu ndio unaoelezwa na methali ya Kiswahili: 'Elimu ni mali.' Elimu ni chimbuko la maarifa muhimu maishani.

Msingi wa utajiri na maendeleo ya binadamu popote alipo basi ni maarifa. Je, maarifa kwa upande wake yana sifa gani? Maarifa yenyewe hayana upinzani. Maarifa uliyo nayo huweza kuwa na watu wengine wengi pasiwe na upinzani baina yenu kwa kuwa kila mmoja ana maarifa sawa. Kila mmoja ana uhuru wa kuyatumia maarifa hayo kama chanzo cha kuyazalisha maarifa mengine. Utumiaji wa maarifa yenyewe hauyamalizi maarifa hayo. Maarifa hayawezi kugusika ingawa mtu anaweza kuyanyumbua maarifa yenyewe kwa kuyatumia kwa namna tofauti.

Maarifa huingiliana na maarifa mengine. Maarifa aliyo nayo mtu mmoja huweza kuhusishwa na maarifa aliyo nayo mtu mwingine ili kuvyaza au kuzuka na maarifa tofauti. Maarifa yanaweza kuchukuliwa kutoka sehemu moja hadi nyingine kwa namna ambavyo mtu hawezi kufanya bidhaa nyingine ile. Kwa mfano, ni muhali mtu kulalamika kuwa hawezi kutembea kutoka sehemu moja hadi nyingine kwa sababu ana mzigo mzito wa maarifa kichwani.

Sifa nyingine muhimu ya maarifa ni kuwa yanaweza kuwasilishwa kwa njia za ishara au mitindo mingine ya kidhahania. Ikiwa unataka kukihamisha chombo fulani kutoka sehemu moja hadi nyingine, lazima uwazie ukubwa wake, uzito wake na labda hata umbali wa panapohusika. Maarifa huweza kubadilishwa au kugeuzwa na kuwa ishara ambazo huyafanya kuwasilishwa kwa njia nyepesi kuliko kwa mfano ikiwa mtu atayawasilisha katika muundo wa, kwa mfano, kitabu.
sambamba au kugotanishwa na kipengele kingine cha maarifa. Huo huwa muktadha mzuri wa kueleweka au kuwa na maana. Kwa mfano, neno 'mwerevu' huweza kuwa na maana kwa kuwekwa katika muktadha wa 'mjinga', 'mjanja', 'hodari' na kadhalika.

Maarifa huweza kuhifadhiwa katika nafasi ndogo sana. Suala hili linaeleweka kwa njia nyepesi tunapoangalia maarifa katika muktadha wa teknolojia. Data zinazowahusu mamilioni ya watu, ambazo zingehitaji maelfu ya maktaba na lukuki ya vitabu, huweza kuhifadhiwa kwenye kifaa kidogo kinachoweza kutiwa mfukoni.

Maarifa hayawezi kudhibitiwa au kuzuiliwa mahali fulani yasisambae. Maarifa huenea haraka sana. Maarifa ni kitu kinachoepuka pingu za watu wanaopenda kuwadhibiti binadamu wenzao. Hata pale ambapo mfumo wa kijamii au wa kisiasa unafanya juu chini kuwadhibiti raia au watu wenyewe, ni muhali kuyadhibiti maarifa yenyewe. Inawezekana kuzidhibiti njia fulani za ueneaji wa maarifa lakini maarifa hayo yatapata upenyu wa kusambaa. Ni kweli kuwa maarifa ni nguvu inayozishinda nguvu zote.

Swali hili lilihitaji mtahiniwa asome kifungu na kusanisi hoja muhimu na kuzifanyia muhtasari bila kuacha mawazo muhimu wala kupoteza maana asili ya kifungu.

Mtahiniwa pia alihitaji stadi ya kutumia viunganishi vifaavyo ili kuleta mtiririko unaoridhisha. Watahiniwa wengi walilemewa katika upande wa kutumia viunganishi ili kutiririsha mawazo. Wengi waliinua sehemu ambazo hazikuwa na uhusiano wowote kihoja. Stadi ya kujieleza kwa mtiririko ufaao lazima ifundishwe.

- Watahiniwa wengi walitatizika katika kudondoa hoja muhimu.

(a) Fupisha aya ya pili na ya tatu. (maneno 55 - 60)

Powered By: www.manyamfranchise.com

Majibu

(a) - Maarifa huyadhibiti maisha ya binadamu
-Maarifa ni nguvu muhimu maishani
-Utajiri na maendeleo hutegemea maarifa
-Maarifa hayana upinzani
-Maarifa hayamalizwi kwa kutumiwa na watu tofauti
-Maarifa hayagusiki

(b) Eleza sifa kuu za maarifa kama zinavyojitokeza kuanzia aya ya nne hadi aya ya nane. (maneno 100 - 110).

Majibu

-Maarifa huingiliana na maarifa mengine
-Huweza kuchukuliwa kutoka sehemu moja hadi nyingine
-Huweza kuwasilishwa kwa njia ya ishara
-Yana sifa ya uhusianaji
-Huweza kuhifadhiwa katika nafasi ndogo
-Hayawezi kuzuiliwa yasisambae.

4.5 MAPENDEKEZO

- Walimu waendelee kuwapa wanafunzi mazoezi ya maswali ya ufahamu na ufupisho na kusahihisha wakizingatia sarufi kwa sababu jambo hili linazingatiwa wakati wa kusahihisha mtihani wa kitaifa.
- Wanafunzi wasisitiziwe kwamba baadhi ya maswali ni ya stadi za juu kama matumizi na tathmini kwa hivyo maswali ambayo hayaonekani kuwa na majibu ya kuinua moja kwa moja huulizwa pia.
- Wanafunzi wapewe mazoezi ya muhtasari huku mtiririko ufaao ukisisitizwa mara kwa mara ili wapate kuzoea kutumia viunganishi kutiririsha hoja katika kujibu maswali ya muhtasari.
- Walimu na wanafunzi watalii maeneo yote ya sajili bila ya kujifunga kwa chache tu ambazo ni za kawaida.

*Masuala yote katika silabasi yafundishwe katika upana wake bila kubagua.

4.6 FASIHI (102/3)

Matokeo ya karatasi ya tatu (102/3) ya miaka ya 2007 hadi 2010.

Mwaka	**2007**	**2008**	**2009**	**2010**
Alama ya Wastani	43.49	31.17	32.72	39.22
Alama ya Tanganisho	13.12	13.64	13.11	14.09

Matokeo ya karatasi ya tatu (102/3 ya mwaka wa 2010 yameimarika kutoka alama ya wastani ya **32.72** mwaka wa 2009 hadi **39.22** mwaka wa 2010.

Tutachanganua swali la kwanza pekee katika karatasi hii kwa sababu lilikuwa la **lazima.** Pia ndilo lililoonekana kuwapa watahiniwa changamoto kidogo.

Swali hili lilikuwa ni **shairi** kutoka diwani ya E. Kezilahabi

Powered By: www.manyamfranchise.com

Soma shairi hili kisha ujibu maswali yanayofuata.

Dhamiri yangu

Dhamiri imenifunga shingoni.
Nami kama mbuzi nimefungwa
Kwenye mti wa utu. Kamba ni fupi
Na nimekwishachora duara.
Majani niwezayo kufikia yote nimekula.
Ninaona majani mengi mbele yangu
Lakini siwezi kuyafikia: kamba, kamba.

Oh! Nimefungwa kama mbwa.
Nami kwa mbaya bahati, katika
Uhuru kupigania, sahani ya mbingu
Nimeipiga teke na niigusapo kwa mdomo
Mbali zaidi inakwenda na siwezi tena
Kuifikia na hapa nilipofungwa
Nimekwishapachafua na kuhama siwezi.

Kamba isiyoonekana haikatiki.
Nami sasa sitaki ikatike, maana,
Mbuzi wa kamba alipofunguliwa, mashamba
Aliharibu na mbwa aliuma watu.
Ninamshukuru aliyenifunga hapa
Lakini lazima nitamke kwa nguvu
"Hapa nilipo sina uhuru!"

(E. Kezilahabi)

(a) Taja mambo manne ambayo mshairi analalamikia.

(b) Kwa nini mshairi haoni haja ya yeye kuwa huru?

(c) Eleza maana ya mshororo ufuatao kama ulivyotumiwa katika shairi.
"Kamba isiyoonekana haikatiki."

(d) Taja na utoe mifano ya aina mbili za tamathali zilizotumika katika shairi hili.

(Q 1a
Majibu
(a) -Kufungwa
-Kunyimwa uhuru
-Alipofungwa pameharibika
-Angependa kuhama lakini hawezi
-Kuna majani mengi mbele yake lakini hawezi kuyafikia

(b)
amekwisha zoea hali yaki
-Hapendi kuonekana tofauti. Hataki kuukosa utu kwa sababu amefungwa katika kamba ya utu.
majibu
(c) Ni dhamiri katika nafsi yake ambayo ameshikilia ambayo haionekani kwa macho ndiyo iliyomfunga

Powered By: www.manyamfranchise.com

Majibu

(d) (i) Tashbihi -kama mbuzi
-Kama mbwa

(ii) Istiari/sitiari -Sahani ya mbingu, kamba isiyoonekana

(iii) Tasfida - Nimekwishapachafua

Majibu

(e) Mishata: Mishororo ambayo maana yake inakamilika katika mshororo unaofuata

Mf: Nami kwa mbaya bahati, katika uhuru kupigania kamba ni fupi na nimekwishachora duara.

Nami kwa mbaya bahati, katika
Uhuru kupigania, Sahani ya mbingu
Nimeipiga teke na niigusapo kwa mdomo
Mbali zaidi inakwenda na siwezi tena
Nami sasa sitaki ikatike maana
Mbuzi wa kamba alipofunguliwa, mashamba

Majibu

(f) Nimefungwa kama mbwa na kwa bahati mbaya katika kutaka kuondoka pale nimeipiga teke sahani ya mbingu ambayo imeenda mbele na siwezi kuifikia.
Na pale nilipofungwa ni pachafu ila siwezi kupatoka.

4.7 MAPENDEKEZO

- Walimu wafundishe vitabu vilivyoteuliwa kwa ukamilifu wake huku wakizingatia ploti,wahusika,maudhui,mbinu na lugha.
- Wanafunzi wahimizwe kutambua masuala muhimu yanayojitokeza katika hadithi zote katika Mayai Waziri wa Maradhi na Hadithi Nyingine
- Wanafunzi wawekewe misingi bora katika fasihi simulizi tangu kidato cha kwanza.
- Walimu wawafundishe wanafunzi wao istilahi muhimu zinazohusiana na ushairi.

* Katika karatasi hii, swali lililohepwa na baadhi ya watahiniwa ni nambari tatu.
Swali hili lilihitaji watahiniwa waweze kukumbuka ni wapi dondoo hilo linapopatikana kitabuni.

TANB. Ni dhahiri kwamba kwa jumla matokeo ya mtihani wa somo la Kiswahili yameimarika katika mwaka wa 2010 yakilinganishwa na mwaka wa 2009.
Ni matarajio yetu kuwa walimu na wanafunzi watamakinika kujifaidi na mapendekezo tuliyoyatoa katika ripoti hii ili kuzidi kuboresha matokeo ya somo la Kiswahili katika siku za halafu.

Powered By: www.manyamfranchise.com